BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE, HABARI NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA NAMB.4 YA MWAKA 1986 NA KUTUNGA SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA YA MWAKA 2018 AMBAYO INAWEKA UTARATIBU WA UUNDAJI NA UENDESHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kwa mara nyingine tena kukutana hapa katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unaoendelea. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani, utulivu, usalama na mshikamano, mambo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Mimi binafsi na Kamati yangu tunaendelea kukushukuru wewe binafsi kwa busara zako, pamoja na wasaidizi wako kwa Kuliongoza vyema Baraza hili katika kufanikisha malengo tuliyojiwekea. Nidhahiri kabisa kwamba, heshima na busara zako ndio moja kati ya siri kubwa ya mafanikio

yanayopatikana katika Baraza hili. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima, busara na nguvu katika kazi yako ya kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 84(7) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2016 , ambayo inayotoa fursa kwa Kamati iliyopelekewa Mswaada kutoa maoni yake kuhusiana na Mswaada husika kadri inavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati inapongeza na kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kufikiria wazo zuri na lenye tija la kuwa na sheria bora itakayoweka muundo imara na usimamizi bora wa Vyama vya Ushirika, kwa lengo la kuongeza misingi imara ya usimamizi, uaminifu, uwazi, na uwajibikaji ili hatimae kupata vyama madhubuti vitakavyokidhi malengo na mahitaji ya wanachama wake, jamii na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lengo na dhamiri ya Ushirika ni kuleta Maendeleo kwa kushirikiana, na katika kutekeleza dhana hii, watu huungana kwa kuunganisha nguvu zao kwa pamoja na hatimae kuunda chama cha Ushirika kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, au shughuli ya biashara

inayomilikiwa kwa pamoja. Aidha wanajamii hujikusanya kwa pamoja kwa ajili kuanzisha chama cha ushirika wa aina mbali mbali kulingana na mahitaji na madhumuni waliojipangia.

Mheshimiwa Spika, tafiti mbali mbali zinaonesha kwamba, dhana hii ya Ushirika hapa kwetu Zanzibar imefanikiwa kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita, licha ya Changamoto kadhaa zilizoikumba sekta hii, jambo ambalo baadhi ya wanajamii walikosa imani na vyama walivyovianzisha kutokana na usimamizi na uendeshaji wa vyama hivyo

Hata hivyo, kwa sasa imani kwa Vyama vya Ushirika imeongezeka, na Vyama vingi vinaendelea kuundwa hasa vile vya Kuweka na Kukopa (***Savings and Credit Co-operative Society*** yaani **SACCOS**). Hivyo ni matumaini ya Kamati kwamba, Kutungwa kwa Sheria hii mpya kutasaidia sana, katika kufikia dhamira nzuri ya serikali ya kuimarisha sekta hii ya Ushirika ikiwa ni njia moja wapo ya kuleta mabadiliko miongoni mwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Ushirika umegawika katika ngazi tatu, yaani Chama cha Msingi, Chama cha Kati na Chama Kikuu Cha Ushirika, ambapo

kwa ujumla Muundo mzuri wa vyama vyote hivyo unategemea uimara wa chama cha msingi cha Ushirika. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha vyama imara vya msingi vinaanzishwa badala ya kukimbilia kuanzisha vyama vya Kati na Vyama Vikuu vya Ushirika. Kwa kuzingatia hilo, Kamati inashauri kwamba, msisitizo zaidi usiwekwe kwenye uanzishwaji wa vyama Vikuu vya Ushirika, lakini kuwepo na uwezeshaji wa wanachama katika vyama vya msingi kwa lengo la kuunda chama imara cha msingi .

Ni matumaini ya Kamati kwamba, tukiwa na Vyama imara vya Msingi , Vyama hivi zinaweza kuunda chama Kikuu cha Ushiriki kilicho imara zaidi.

Kamati inaamini kwamba, lengo la kuwa na Vyama imara vya Msingi litatimia kama juhudi za makusudi za kuimarisha vyama vya msingi vya zamani na vipya vitakavyoanzishwa kwa kuwapa taaluma kwa lengo la kuongeza wanachama wake, uwajibikaji na uaminifu wa viongozi wao jambo ambalo litaongeza demokrasia katika maamuzi yanayohusu uendeshaji wa vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile tukiwa tunaelekea kuupitisha Mswaada huu, tunamshauri Mheshimiwa Waziri kujipanga Vizuri pamoja na wataalamu wake, kuvisimamia ipasavyo vikundi vya wajasiriamali walioamua kushirikiana katika

kukabili tatizo la kiuchumu katika jamii kwa kuimarisha misingi ya ushirika ikiwemo uanachama wa hiari, uongozi wa Kidemokrasia, mgao wa ziada kufuatana na jinsi mwanachama alivyochangia , elimu ya Ushirika , ushirikiano baina ya vyama vya Ushirika na kuijali jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu na ubora wa Mswaada huu ambao baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais itakua Sheria itakayosimamia Vyama vya Ushirika , Kamati yangu inawasisitiza wananchi kuzidi kuunda vikundi vya Ushirika ikiwa ni miongoni mwa ving'amuzi vitakavyobadilisha hali ya maisha na kupambana na umasikini kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu Katika mizunguko ya kazi za Kamati pia tumebaini faida kubwa zinazopatikana kwa wananchi wetu walioamua kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Msingi ikiwemo;-

1. Wanachama wengi wananufaika kwa kutunza fedha zao kama amana na akiba kwa salama.
2. Kutanua wigo mkubwa wa bidhaa kwani wanachama hupata mikopo ya kiuchumi, kijamii na dharura.

3. Vyama vya Ushirika vinaisaidia kuikwamua jamii kuondokana na umasikini ikiwemo kumudu gharama za masomo kwa watoto wao, kujenga nyumba bora za kisasa, kumudu kununua vyombo vya usafiri , kuanzisha miradi ya kibiashara , pamoja na kupata uwezo wa kukidhi mahitaji muhimu ya kibinadamu ikiwemo chakula na matibabu.
4. Kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii imekipitia na kukitafakari kwa makini Kifungu cha 5 (1) cha Mswaada huu kinachoelezea Kazi za Idara ya Maendeleo ya Ushirika. Kamati pamoja na kuridhika na Kazi na majukumu mbali mbali ya Idara hii hasa yale ambayo yameainishwa katika kifungu hiki hasa Kifungu cha 5(1) (c) ambacho pamoja na mambo mengine kinaweka masharti na Kinaipa mamlaka Idara hiyo kusajili aina zote za vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inakubaliana na kuunga mkono uamuzi huu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuhamisha shughuli za Usajili wa aina zote za Vyama vya Ushirika kutoka Wizara ya Biashara na Viwanda zilizokua zinazofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, na badala yake

jukumu hilo sasa liachiwe Idara ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake, na Watoto.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara zetu za Kamati mara kadhaa tulipokuwa tukitembelea vikundi vya Ushirika Unguja na Pemba, pamoja na mambo mengine Kamati imegundua kwamba Shughuli za Vyama vya Ushirika zinahitaji taaluma na huduma kubwa za vyama ikiwemo kuratibu, ushauri wa misingi ya uanzishaji, Kanuni za Uendeshaji , Uongozi na Kujenga Mitaji. Aidha baada ya Usajili wa Vyama vya Ushirika vinahitaji huduma za kitaalamu ikiwemo Katiba imara, mipango ya biashara , matarajio na jinsi ya Kuendesha Mikutano. Utaalamu huu mara nyingi hupatikana kutoka kwa wataalamu na Maafisa wetu wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia inasisitiza kwamba jukumu hili la usajili Vyama vya Ushirika kubaki Idara ya Maendeleo ya Ushirika, kwani tunaamini kwamba, litapunguza muda wa ufuatiliaji, gharama za usajili na pia kupunguza usumbufu uliokuwepo hivi sasa, ukizingatia ya kwamba usajili wa vyama vya Ushirika chini ya Wakala wa Biashara na Mali unafanywa kwa njia ya Mtandao

ambapo mara nyengine huleta usumbufu mkubwa kwa sababu ya ukosefu wa taaluma kwa wanaushirika wetu ambao wengi wako vijijini.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaamini kwamba kuipa mamlaka ya kusajili Vyama vya ushirika Idara ya Maendeleo ya Ushirika kutaondosha utata uliopo wa utoaji wa maelekezo ya kisheria kwa Vyama vya Ushirika, kwani kwa utaratibu wa zamani Wanaushirika walilazimika kusajili vyama vyao chini ya Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara, Sheria Namba 12 ya Mwaka 2012 iliyoko chini ya Wizara ya Biashara na Viwanda pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika iliyoko Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Miongoni mwa malengo makuu ya Ushirika ni kuwawezesha wanachama wake, na kama tunavyofahamu masuala ya uwezeshaji yako chini ya Wizara ya ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake, na Watoto. Hivyo Kamati imeshawishika kukubaliana na mawazo ya Serikali ya kuzihamishia shughuli za Usajili wa vyama Katika Idara ya Maendeleo ya Ushirika, ili kurahisishwa mipango ya uwezeshaji wa vikundi hivyo na hatimae viweze kufikia malengo yao waliojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuikumbusha serikali kwamba , kuwa na sheria ni kitu kimoja na utekelezaji wake ni kitu chengine , hivyo basi tunawaomba wale waliopewa dhamana ya utekelezaji wa sheria hii wahakikishe kwamba, wanaifanyia kazi kwa uadilifu hasa kwa yale maeneo yanayogusa masuala ya Utoaji na Ufutaji wa Leseni, Uteuzi wa mfilisi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Aidha, Kamati inaomba hilo liende sambamba na uharakishwaji wa utungwaji wa Kanuni zinazohitajika ili Sheria hii iweze kutekelezeka kwa ufanisi wa haraka na wenye tija kwa wanachama wa vyama hivyo vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imevifanyia marekebisho jumla ya vifungu 28 vya Mswada huu, ambapo takriban marekebisho yote ya vifungu hivyo ilikuwa ni lugha, kufuta ama kuongeza maneno ili kupata mtiririko mzuri wa lugha pamoja na maana iliyokusudiwa. Maelezo kamili ya Marekebisho ya Kamati kuhusiana na Mswada huu, yanapatikana katika waraka wa marekebisho ambao umesambazwa kwenu waheshimiwa wajumbe.

Hivyo basi, Waheshimiwa wajumbe kwa heshima naomba muyapitie kwa uangalifu mkubwa mapendekezo hayo ya Kamati na muyaunge mkono kwa

lengo la kuuboresha Mswaada huu ili hatimae iwe sheria ambayo itatumika kwa lengo la kuleta ufanisi na maendeleo kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nikielekea ukingoni mwa hotuba yangu, nakushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza mbele ya Baraza lako tukufu , na ni matumaini yangu kwamba wajumbe wenzangu watauchangia kwa wingi Mswada huu kwa lengo la kuufanya uwe bora zaidi na hatimae kuupitisha, ili Wizara na serikali kwa ujumla iweze kufikia lengo la kutayarishwa Mswada huu kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuishukuru Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake, na Watoto kwa kuifanyia Kamati pamoja na Wenyeviti wa Kamati zako, mafunzo ya siku moja ya kutujengea uwelewa juu ya Mswada huu. Pia napenda kuwashukuru wadau wote waliofika Mbele ya Kamati na kutoa maoni yao, na tunawambia kwamba , kwa dhati kabisa tunawashukuru na kuthamini sana mawazo yao ambayo yametupa mwangaza mkubwa wa kuuboresha Mswada huu.

Aidha, tunawashukuru wanasheria wa Afisi ya Baraza na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kufanikisha vyema kazi za kuupitia Mswada huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru na kuwapongeza sana wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii kwani ushirikiano wao wa dhati, pamoja na nguvu, ari na hamu ya kufanya kazi bila ya kuchoka , ndizo zilizonipa nguvu mimi na ujasiri wa dhati wa kusimama katika hadhara hii, na kutoa Maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua kwa kuwataja kwa majina wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya wanawake, Habari na Utalii kama ifuatavyo;-

1.	Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mussa Foum Mussa	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Makame Said Juma	Mjumbe
4.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
5.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mjumbe
6.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
7.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
8.	Ndg. Himid Haji Choko	Katibu
9.	Ndg. Mussa Issa Mussa	Katibu
10.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani
11.	Ndg. Azmina Hamad Khamis	Msaidizi

Mheshimiwa Spika, naunga Mkono Hoja.

……

(Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis)

Mwenyekiti,

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake , Habari na Utalii,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.